


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



MWELEKEO WA MVUA ZA *MASIKA MACHI* - MEI 2019



## **Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Masika kipindi cha Machi-Mei 2019**

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua katika kipindi cha Machi - Mei 2019, ushauri na tahadhari kwa wadau wa sekta mbalimbali wanaohitaji taarifa za hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yao kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na wanyamapori, maliasili na utalii, nishati na maji, mamlaka za miji, afya pamoja na menejimenti za maafa. Kwa muhtasari, mwelekeo huo na athari zake unaonesha kuwa:

- i. Katika kipindi cha Machi hadi Mei, 2019 kwa ujumla mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya ukanda unaopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka nchini.
- ii. Mvua za Masika zinatarajiwa kuanza mapema na kuisha mapema na msimu huu unatarajiwa kuwa na vipindi vifupi vya mvua kubwa.
- iii. Katika baadhi ya maeneo vipindi vya upungufu wa mvua vinatarajiwa katika maeneo machache nchini hususan kaskazini mwa mikoa ya Kigoma na Morogoro.

Wakati huo huo, mvua za Msimu ambazo zilianza mwezi Novemba, 2018 zinatarajiwa kuendelea hadi mwishoni mwa mwezi April 2019. Katika kipindi hicho mvua hizo za Msimu zinatarajiwa kuwa za wastani katika maeneo mengi. Hata hivyo, mvua za chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo machache ya kanda ya Kusini ( Ruvuma), pamoja na mikoa ya Dodoma na Singida.

## **(I) MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA KIPINDI CHA MACHI - MEI 2019**

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa ilivyo kwa sasa na jinsi inavyotarajiwa kuwa kwa kipindi chote cha Machi – Mei 2019 (kama ilivyoelezwa katika kipengele II cha taarifa hii), mvua za wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani.

### **1. *Mvua za Masika 2019 (kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua)***

Msimu wa mvua za *Masika* ni mahususi katika maeneo ya Nyanda za Juu Kaskazini-mashariki, pwani ya Kaskazini na visiwa vya Unguja na Pemba, ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Sehemu kubwa ya maeneo haya yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani katika msimu wa Masika 2019. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kaskazini-mashariki, hususan mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, kuna uwezekano mkubwa wa mvua za juu ya wastani.

#### **1.1 *Kanda ya Ziwa Viktoria: (Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Shinyanga):***

Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Februari katika mkoa wa Kagera na kusambaa katika mikoa ya Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Shinyanga katika wiki ya pili ya mwezi Machi, 2019. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo machache ya mkoa wa Kagera na wilaya ya Kibondo, upungufu wa mvua unatarajiwa.

**1.2 Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Morogoro):**


Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya nne ya mwezi Februari hadi wiki ya kwanza ya mwezi Machi 2019, katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba, na kusambaa katika mikoa wa Tanga na Kaskazini mwa mkoa wa Morogoro katika wiki ya kwanza ya mwezi Machi. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo machache ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro yanatarajiwa kuwa na upungufu wa mvua.

**1.3 Nyanda za juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza katika wiki ya nne ya mwezi Februari, 2019. Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Arusha na Kilimanjaro. Aidha, Mashariki mwa mkoa wa Kilimanjaro (Same) na maeneo mengi ya mkoa wa Manyara yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani.

**Mvua za Msimu (Novemba - Aprili) kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka.**

Mvua za *Msimu* zilizoanza mwezi Novemba, 2018 zinaendelea katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (mikoa ya Dodoma, Singida, Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Ruvuma, Lindi, Mtwara na Kusini mwa Morogoro). Mvua hizi zinatarajiwa kuwa za wastani katika maeneo mengi, wakati mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo ya kati ya nchi (mikoa ya Dodoma na Singida) na yale ya Kusini (mkoa wa Ruvuma).



*Picha 1 – Ramani ya wastani wa mvua – kulia: Wastani wa muda mrefu wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba; Kushoto: Mwelekeo wa mvua katika msimu huu wa Machi hadi Mei 2019.*

**Angalizo:**

*Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza pia katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani na chini ya wastani.*

**(II) MIFUMO YA HALI YA HEWA**

Hali ya joto la bahari la juu ya wastani ambalo limerekodiwa katika maeneo ya kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi inatarajiwa kuendela katika kipindi chote cha Machi-Aprili-Mei. Hii inatarajiwa kudhoofisha upepo kutoka Mashariki kuelekea katika pwani yetu na hivyo kupunguza mvua katika maeneo haya. Joto la juu ya wastani katika Bahari ya Hindi linatarajiwa kuongeza uwezekano wa matukio ya vimbunga katika maeneo ya kusini-mgharibi mwa Bahari ya Hindi. Kwa upande mwingine, joto la wastani linatarajiwa kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) na hii inatarajiwa kupunguza msukumo wa upepo wenye unyevunyevu kutoka katika misitu ya Kongo. Aidha, pamoja na uwepo wa joto juu ya wastani katika eneo la kati la kitropiki la Bahari ya Pasifiki, mchango wake katika mvua nchini kwa kipindi cha Machi-Aprili-Mei, 2019 unatarajiwa kuwa hafifu.

### **(III) ATHARI NA USHAURI**

#### **Kilimo na Usalama wa Chakula, Mifugo na Wanyama pori**

Katika maeneo ambayo yanatarajiwa kupata mvua za juu ya wastani hadi wastani, hususan maeneo ya nyanda za juu Kaskazini-mashariki (mikoa ya Arusha na Kilimanjaro), mvua zinatarajiwa kunufaisha uzalishaji wa mazao ambayo yanastahimili unyevunyevu mwingi ardhini. Sekta ya uvuvi, katika maeneo haya, inaweza kuathiriwa kutokana na wingi wa mtiririko wa maji katika mabwawa ya samaki na hivyo wafugaji wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki. Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani, shughuli za kawaida za kilimo zinatarajiwa. Kwa upande mwingine, malisho na maji ya kutosha kwa ajili ya mifugo na wanyamapori vinatarajiwa.

#### **Nishati, madini na Maji**

Upatikanaji wa maji unatarajiwa kuimarika, hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za juu ya wastani hadi wastani. Kina cha maji katika mabwawa na mito kinatarajiwa kuongezeka. Hata hivyo, athari katika miundombinu ya rasilimali maji inaweza kujitokeza. Shughuli za uchimbaji madini katika migodi midogomidogo zifanyike kwa kuzingatia tahadhari zinazotolewa kwani ongezeko la maji katika udongo linaweza kusababisha maporomoko ya ardhi.

#### **Mamlaka za Miji**

Huduma za maji safi na maji taka zinaweza kuathirika, hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za juu ya wastani hadi wastani. Mamlaka za miji pamoja na wananchi wanashauriwa kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa mifumo na njia za kupitisha maji zinafanyakazi katika kiwango cha kutosha ili kuepusha maji kutuama na kupelekea mafuriko na athari nyingine.

### **Sekta ya Afya**

Kwa kuwa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za kutosha, milipuko ya magonjwa ( kwa mfano: kipindupindu, kuhara, homa ya matumbo nk) inaweza kujitokeza mara kwa mara. Hivyo ushauri unatolewa kwa mamlaka husika na jamii kuchukua hatua stahiki kupunguza athari za kiafya zinazoweza kujitokeza.

### **Menejimenti ya Maafa**

Kutokana na mvua za kutosha katika maeneo mengi, mafuriko na athari nyingine zitokanazo na mvua nyingi vinaweza kusababisha uharibifu wa makazi, miundombinu na upotevu wa mali vinayoweza kusababisha kuumia au kupoteza maisha. Kwa hiyo, menejimenti za maafa, watoa huduma za dharura pamoja na wadau wengine wanashauriwa kuchukua hatua za kuweka mipango stahiki kuhakikisha utayari wa kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza.

### **Vyombo vya habari**

Ushauri unatolewa kwa vyombo vya habari kufuatilia mara kwa mara na kusambaza taarifa sahihi za mienendo ya hali ya hewa na mirejeo inayotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA). Wanahabari wanashauriwa kutafuta na kutumia maelezo ya wataalam wa sekta husika katika kuandaa na kufikisha taarifa za masuala mtambuka ya hali ya hewa kwa jamii.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendeleo kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

*Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.*

**Mamlaka ya hali ya hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa za mwelekeo wa mvua nchini.**

Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania:

Dkt. Agnes L. Kijazi  
**MKURUGENZI MKUU**